

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
 ISO 9001:2015 CERTIFIED



**KUONGEZWA KWA MUDA WA KUTUMA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI
 ZA MAUDHUI (UTANGAZAJI WA KIBIASHARA – REDIO) KUTOKA TAREHE 20 DESEMBA 2022
 MPAKA TAREHE 19 JANUARI 2023 KWA MAENEO YALIYOAINISHWA HAPA CHINI**

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 ili kusimamia mawasiliano ya kielektroni na huduma za posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na huduma za utangazaji kwa upande wa Tanzania Bara.
2. Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za maudhui ya redio (Matangazo ya Kibiashara – Redio) limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

Mkoa	Eneo la Huduma	Kiasi cha Masafa Yaliyopo
Njombe	Njombe	1
	Ludewa	2
	Wanging'ombe	2
	Makete	2
	Makambako	2
Kagera	Missenyi (Mutukula)	1
	Biharamulo	1
Simiyu	Bariadi	2
	Itilima	2
Mtwara	Mtwara	1
	Masasi	2
	Tandahimba	2
	Newala	2
Singida	Manyoni	1
	Ikungi	1
	Mkalama	1
	Iramba	1
Rukwa	Sumbawanga Rural	2
	Kalambo	2
	Nkasi	2
Manyara	Hanang	2
	Kiteto	2
Ruvuma	Mbinga	1

Mkoa	Eneo la Huduma	Kiasi cha Masafa Yaliyopo
	Nyasa	1
	Tunduru	1
	Namtumbo	1
Lindi	Nachingwea	1
	Kilwa	1
	Mtama	1
	Liwale	1
	Ruangwa	2
	Mkinga	1
Mara	Musoma Town	1
	Rorya	1
Tabora	Tabora Municipal	2
	Igunga	1
	Nzega	1
Katavi	Mpanda	2
	Nsimbo	2
	Mlele	2

3. Waombaji wanatakiwa kuzingatia mwongozo wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: <https://www.tcra.go.tz/uploads/documents/sw-1665384791-Mwongozo%20kwa%20Waombaji%20-%20ITA%207%20Oktoba%202022.pdf>
4. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kwa kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao **Tanzanite Portal** kupitia kiunganishi kifuatacho: <https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm> kabla ama ifikapo tarehe **19 Januari, 2023**.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
Mawasiliano Towers,
20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P. 474,
14414 DAR ES SALAAM.